Tuzungumze

Wazee wetu wachungwe !

Kwa sasa hapa mjini ukavu, ukitembea mikoa- i na kandokando za mji, tapigwa na bumbuazi kiwakuta wazee hasa hao alioachishwa kazi waki- unjamia mtungi wa chi- uku (musululu), kasi- isì na vichupa vya ka- yanga wanaotaja "adju- nt Masirika,. 12 volts hajue mkwe." Na wengi ti yao hushikwa hasa magonjwa ya maini, ridi yabisi (rhumatisme), wa bofu la tumbo (estomac) na kazalika. Hayo yote yatokana na ukosefu wa matunzo kulingana na hali ya sasa.

Kwa kweli tukitizama kwa karibu, hali ya wazee wetu wa leo ya kuwa mbovu kwani baada ya kupumzishwa na shirika ao kazi za serikali waliokuwa wakitumikia pato lapunguka na hata mara moja moja nusu ya feza wanaotumiwa na chuo chenyi kuhusika na usalama wakijamii nchini (INSS) haiwafikie. Ni hivi hukosa hata sabuni navinginepo vya lazima kwa kuulinda mwili wao sawa zamani walipokuwa kazini.

Kwa kuwa Baba wa Taifa, Mareshali Mobutu, alisisitiza sana kama mpango wa kijamii ya... utowe matunda mazuri siku za usoni na kati yao machungo mema ya wazee, kwa hiyo yaombwa kwa wakuu wa mji wa Bukavu kama vile wa jimbo; wawajitatanue kutafuta majawawabu kwa kuepusha wazee wetu hali hiyo. Kama vile kuwatafutia nafasi ya mapumziko wakisoma vitabu, masimulizi kati yao, nyumba ya michezo na maburudiko kazaa wa kazaa. Pahali ya kuwaachilia kufyonza mvinyo mchana kutwa na kujilevya wakidoweadowea malofu kama mabata mikoani wasipojua lakufanya.

Ombi hilo lisikilike kwani ni hatari siku zijazo hakutakuwako tena wazee walinda mila na mbinu zetu. Basi tuseme wazee wetu wachungwe ginsi inavyofaa kisha kuachishwa kazi. Mapumuziko yawe bora.

Bisimwa L.-B. Tserou.

JUA

Gazeti la Kivu

Mwaka wa 12 nº 277 Tarehe 8 mpaka 14 Juni 1985

Kiongozi : Mutiri - wa - Bashara.

Kwako Bibi

Nyama ya kuku imeruhusiwa sasa ?

Katika mahali mengi ila ya mababu ili wakaaza kabisa wanawake kua nyama ya kuku, nyama ma samaki fulani fulai. Lakini leo hii utaakuta kina mama, bibi a dada huvunja mfupa a kuku kama fisi baada a kusakanya minyofu na gali, ndizi, wali na inginepo. Je; kwa nini abadiliko hayo yote ?

akati tulikuwa katika asimulizi na wasichana wabinti), mama na bibi ulani fulani, wao husea kuwa mila hiyo ya maabu ilikuwa ya kumuonea, umtia kweli mke katika tumwa ama chini ya kiningino. Ilikuwa ni roho na ulafi wa mme wani nyama ya kuku inao "vitamini na proteii" kwa kujenga mwili. wa hiyo hatusikii kwa ini wanaume wazamani alikuwa wakikataza wake ula vyakula vya aina ulani, ila kwa kuwa, semavyo mungwana, haba a haba hujaza kibaba, anawake walianza kuonja chuzi, kula yayi na wishoe kula viumbo mbaimbali hata firingisi finyango) kiumbo kinahowekwa kwa mme tu.

Kunako vilabo ama kweyi ma hoteli nyama ya kuku yapigwa, huchomwa hukaangwa na kutolewa kwa wanawake ao wanaume kila mmoja ginsi atamani.

kulingana na mafasirio yaliotolewa na wababa, wao husema kuwa hali hiyo yatokana na ukosefu wa vyakula kwani hapo zamani vyakula kwa ujenzi wa mwili vilikuwa vya kutoshelea na vya mitindo nyingi kama vile, maziwa, mtama, mihindi, ndizi, kalanga, mhogo, nyama, maharagi na maboga kazaa wa kazaa. Lakini leo hii, mshahara ni mdogo, mavuno ya shamba madogo pia na labda watu hawana hata shamba lile, mawindo na uvuvi hayafanyike tena kama inavyofaa.

Kumbe hali ya feza na uchumi katika maisha ya leo yasukuma watu kuvunja vizila na mila fulani fulani. Kutokana na hali hiyo ya ukosefu wa vyakula kwa ujenzi wa mwili, wanawake waruhusiwa sasa kula nyama ya kuku kwani maziwa ya mama ndiyo chakula cha kwanza na cha lazima kwa watoto wachanga. Na maziwa hayo yafaa yawe na viungo vyote vya lazima.

Bisimwa L.B. Tserou.

Je umesikia ... ?

KAMA huyo makamu wa mwenyekiti wa mtaa wa Bagira, mwananchi A.S... ingawa alipigwa bakora ya kimapinduzi na kuachishwa kazi kwa muda, alijiruhusu kulipisha feza na kuomba vyakula kazaa kwenyi soko moja ya mtaa wake.

Kwa bahati mbaya alishikwa mkono chunguni na askari jeshi na kupelekwa kwenyi korti la askari jeshi. Huko kwa utundu wake alisagwa konde na hata kupoteza jino moja.

Ebu kumbe chupa muliokuwa chumvi hamuishe utamu na mkula pupa alipa ulafi wake kwa... ?

KWAMBA kunako vyuo vyenyi kuongozwa na F.M., ili ukubaliwe yafaa uwe ngambo ya mto R ao ufanane... Na zaidi ya hayo yafaa kuonyesha vikartasi vya utambulisho na kusumulia lugha ya... Eti panya za kizungu za juana kwenyi mikia. Na kisha kutubu makosa yake amerudishwa kazini.

Baada ya mkusanyo wa shirika la akiba na mkopo

SUNGURA KALIA MACHOZI, BISIMWA KASAGA MENO

Kunako chuo cha Ibanda mjini Bukavu, mnamo tarehe 1 juni 1985, wajumbe wa wanamemba wa Shirika la akiba na mkopo (COOCEC) walikutana katika mkusanyo wao mkuu.Baada ya uchunguzi muhimu uliofanyika, ilionekana kuwa mambo hayakuwa yanaendeka barabara kulingana na mwelezo wa mahitaji ya wanamemba na wataalam katika ulinzi wa feza, uchunguzi ukiwa wa reja reja na usio halali kama inavyofaa kutokana na uhuru wa mashirika madogomadogo, uhuru ambao ulifikilia uasi (indiscipline) na kutia fujo shirikani.

KUNA NINI KATI YA VIONGOZI NA SHIRIKA?

Mpaka hapo mambo yalikuwa yakitezamiwa kuongoka vizuri. Lakini walipofikilia kitambo cha feza, ubongo wa watu ukaanza kuyeyuka kama mafuta ya kambili. Kwani ımafasirio› yaliyotolewa na viongozi wa shirika hilo hayakuweza kusadikiwa na wajumbe wa mashirika madogo madogo yapata 22 jimboni.

Kisha kutolewa mafasirio muhimu juu ya matumizi na mkopo wa feza na wataalam kazaa, ilionekana wazi kuwa feza nyingi zilipokonywa na prezidenti wa shirika hilo mwananchi Sungura na makamu wake mwananchi Bisimwa ambao wapashwa feza za kutosha kwa shirika. Mwanachi Sungura alipashwa zaīre 83.000, lakini wakati aliposikia kama mkusanyo mkuu utafanyika akajipigapiga na kutoa tu kiasi cha zaīre 55.000 akisahau faida za pesa hizo yapata zaire 28.000. Ila kwa kuwa siku za mwizi ni arubaini, akaingia katika mtego na makamu wake, mwananchi Bisimwa apashwa kiasi cha zaire 150.000.

Kwani nyumba alizozipana rehani kwa mkopo wa feza hizo hazifai. Na muda wa kurudisha pesa hizo ulikuwa umetimu. Sasa hapo wakorofi hao hulia machozi ya uchungu na kusaga meno wakijuta kilichowatuma kusakanya feza za umma. Tutawajulisha kuwa siku si nyingi mwananchi Sungura kashitakiwa juu ya upokonyaji wa feza za koperative ya mtaa wa Kadutu. Na leo hii ujanja wao kama wa "sungura mjanja" ulivumbulika.

UCHAGUZI

Baada ya uchaguzi na mafasirio yaliyotolewa kwa wanamemba, hawa waliamua ni bora wajipatie viongozi vipya. Kwa hivi, mwananchi Bazirunguka Naweza mjumbe wa koperative ya Idjwi kamgomboa mwananchi Sungura na mwananchi Bulambo kawachiliwa kiti na mwananchi Katwanyi kunako uakili (commission) wa mkopo unaoongozwa na mwananchi Mutula kwa sasa.

Kwa ngambo ingine, yajulishwa kuwa koperative ya Butembo ilijitenga na mengine na kuunda shirika lake pekee liitwalo shirika la feza nchini Zaīre (Cofiza).

BISIMWA L-B. Tserou.

SHAIRI

Sala kwa hela

oooooo Hela
ama Franka
Pesa, Makuta
nakusalimu

Mchana kutwa
Na usiku
nakuwaza
Ni wewe
mama na bab'angu
ni wewe

Kwani
mfukoni mwangu
unaleta raha
mkononi mwangu
unaleta furaha
machoni mwangu

Ni hivi
duniani kote
kila mtu
anakuwaza wewe
anakutafuta wewe
anakuabudu wewe
Kwani husema
bila wewe
ni magumu
ni mateso
ni masumbuko

Kwa hiyo
nakusihi hela
uje, ujionye
unijaze mifuko
siku zote

Nipate vyote
nisikose kitu
niishi vema
milele na milele
Amen.